

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kwanza – Tarehe 8 Novemba, 2011

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

KIAPO CHA UTII

Wajumbe wafuatao waliapa Kiapo cha Utii na kukaa katika nafasi zao ndani ya Bunge:-

Mhe. Mohammed Said Mohammed  
Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu

**MBUNGE FULANI:** CCM oyee! (*Makofi*)

TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Bunge wa Nne pamoja na Muswada wa Sheria ya Fedha (*The Finance Bill 2011*), ambao nilikwishautolea taarifa kwamba, ulikwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria ya Nchi, Bunge lilipitisha Muswada mmoja wa Sheria ya Serikali uitwao *The Appropriation Bill, 2011*. Mara baada ya kupitishwa na Bunge na baadaye kupitia katika hatua zake zote za uchapishaji, Muswada huu ulipelekwa kwa Rais ili upate kibali chake.

Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba, Muswada huo ulikwishapata kibali cha Rais na kuwa Sheria za Nchi uitwao *The Appropriation Act, 2011*, Na. 6 ya Mwaka 2011.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na Muswada huo tu na umepitishwa na kupewa kibali cha Rais. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tulipokuwa tumeatumzika, Bunge tulipata maafa makubwa sana ya meli kupinduka kule Zanzibar, ninaomba tusimame tuwakumbuke wahanga wote waliofariki katika ajali ile.

(Hapa Wabunge wallisimama kwa dakika moja kuwakumbuka Wahanga wa ajali ya Meli ya MV Spice Islander)

**SPIKA:** Roho zao zipumzike mahali pema mbinguni. *Amina.*

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Utaratibu na Utekelezaji wa Ahadi za Mheshimiwa Rais

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais anapokuwa katika ziara zake za kutembelea Wananchi na kukagua au kufungua Miradi ya Maendeleo huwa anakutana na majukumu ya papo kwa papo na kuyatolea ahadi ili yaje kutekelezwa:-

- (a) Je, ni Wizara/Idara gani inayoratibu utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais?
- (b) Je, inafuatilia kwa ukamilifu utekelezaji wa ahadi hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri wa Mkuu, ndiyo yenyeye jukumu la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi mbalimbali za Mheshimiwa Rais, zinazotolewa kwa Wananchi kila anapofanya ziara ya kikazi mikoani. Aidha, jukumu hilo linaenda sambamba na uratibu wa utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Baadhi ya ahadi ambazo ni za moja kwa moja zinazoshughulikiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Rais mwenyewe na zile zinazohitaji bajeti, huwekwa kwenye Mipango ya Wizara au Mikoa husika kutegemeana na aina ya ahadi.

(b) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, inafuatilia kikamilifu ahadi hizo ambazo hutolewa katika Wizara na Mikoa na kuchapishwa Kamusi Maalum ambazo Waheshimiwa Wabunge wote walipewa ili iwe rahisi kwa ufuatilaji na Wizara na Mikoa huwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, taarifa ya utekelezaji wa ahadi hizo kwa kadiri zinavyotekelzeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba niishukuru Serikali kwa kutekeleza ahadi ya Rais ambayo alitoa kuhusiana na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo na sasa imeanza kujengwa.

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Pachani – Lusewa ili iwe inapitika kikamilifu mwaka mzima lakini ahadi hiyo hajatekelezwa; na kwa kuwa kuna ahadi ambayo bado hajatekelezwa ya kukipa hadhi Kituo cha Afya Kilichopo kilomita zaidi ya 260 kutoka Makao Makuu ya Wilaya kiwe na *theatre* na huduma ambazo angalau zinapanana na Hospitali ya Wilaya; na kwa kuwa kuna ahadi ya *solar* na kompyuta kwenye *SACCOS* iliyopo katika Kata hiyo ya Lusewa; je, Ofisi ya Waziri Mkuu inaweza kusimamia utekelezaji wa ahadi hizo?

**SPIKA:** Ahsante. Ninaomba maswali yaye mafupi ili tuweze kuwapa nafasi na wengine.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi katika maeneo mbalimbali wakati wa kampeni, lakini pia ahadi nyingi zipo kwenye llani kama nilivyosema na nyingine alizitoa wakati akifungua Bunge la Kwanza hapa ndani. Mtakumbuka wakati wa Bunge la Bajeti, Ofisi yangu iliwapeni vijitabu vitatu; kimoja

kinaonesha ahadi za Mheshimiwa Rais; uchambuzi wa ahadi alizozitoa hapa Bungeni kupitia Hotuba yake; na Kamusi ya Utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndiyo Chama Tawala. Ahadi nyingine ndiyo kama hizi anazozungumza Mheshimiwa Kawawa zilizotolewa katika mikutano na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuwathibitishia Mheshimiwa Kawawa na Waheshimiwa Wabunge kwamba, ahadi zote zimerekodiwa na zinatekelezwa na Wizara zinazohusika na Mikoa na Ofisi yake, kwa mujibu wa Kalenda ya Bajeti. Ahadi hizi nyingi zimetolewa mwaka jana na kipindi kilichotolewa ahadi ni hiki cha muhula wa miaka mitano.

Kwa hiyo, ninataka kumfahamisha Mheshimiwa Kawawa kwamba, ahadi zote sisi tunazo na tunaamini wa nia njema aliyoahidi katika kipindi cha miaka mitano cha kipindi chake cha mwisho, ahadi hizi *Inshallah* zitatekelezwa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa kuwa ahadi za kutekeleza Miradi ya Maendeleo za Mheshimiwa Rais zipo nchi nzima; na kwa kuwa ahadi hizi hazina ratiba maalum kwamba zitatekelezwa mwaka fulani na mwaka fulani; na kwa kuwa Wabunge wanapata shida sana kujibu maswali hayo kwenye mikutano kwenye Majimbo yao. Je, Serikali haioni sasa kuna kila sababu ya kuainisha ahadi zote na kuzipa tarehe kwamba ahadi fulani itatekelezwa mwaka 2012 na ahadi fulani mwaka 2014 ili kuondoa usumbufu kwa Wabunge kuhojija na Wananchi kwenye mikutano yao? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, wazo allolloita ni zuri na hata ukiangalia Kitabu chetu cha Kamusi tulichopanga nia yetu ni hiyo, ndiyo maana tumeainisha, tumezichambua na tumezipanga na kuzisambaza katika taasisi zinazohusika ili zitekelezwe kulingana na vipindi vitano vya bajeti. Vilevile tunaendesha kwa *cash budget*, hatuwezi kupanga kabisa kwamba ni lazima itekelezwe, lakini ukisoma ile ratiba iliyomo kwenye Kamusi imepanga vipaumbele vyote vya ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais katika kipindi chote cha miaka mitano. Kwa hiyo, ratiba ni miaka mitano.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Mwaka jana haikuwa kipindi cha kampeni, tarehe 15 Mwezi wa Nane, Mheshimiwa Rais aliahidi katika Kituo cha Kipatimo kwamba atasaidia kutoa pesa kwa ajili ya ufunguaji wa mashine ya *X-Ray*; Waziri pamoja na majibu yako sikubaliani kwamba tutakaa miaka mitano tukisubiri *X-Ray machine* wakati Wananchi wanapata matatizo; ni lini ahadi hii itatekelezwa? Ahsante.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ahadi hiyo Mheshimiwa Rais aliahidi na mimi ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mangungu kwamba, tupo katika utaratibu wa kutimiza au kutekeleza ahadi hiyo ya Rais.

Na. 2

#### **Kituo cha Afya cha Muhoro Kupatiwa Gari la Wagonjwa**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Wakati anawasalimia Wananchi wa Muhoro kwenye Sherehe za Uwekaji wa Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Barabara ya Ndundu – Somanga, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kuwa Kituo cha Afya cha Muhoro kitapatiwa gari la kubebea wagonjwa: Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais aliahidi kutoa Gari la Wagonjwa mwezi Septemba, 2009 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Muhoro kilichopo katika Halmashauri ya

Wilaya ya Rufiji. Serikali imeteketeza ahadi yake iliyotolewa na Mheshimiwa Rais kwa kupeleka gari aina ya *Land Cruiser Hardtop* lenye Namba ya Usajili SM 9042, mwezi Aprili, 2011. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kuititia Timu ya Uendeshaji wa Shughuli za Afya ya Wilaya, iliamaa kupeleka gari hilo katika Kituo cha Afya cha Kibiti ambacho kilipandishwa hadhi ili kutoa huduma za dharura na kipo umbali wa kilomita 90 kutoka Utete.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ina magari matatu ya kubebea wagonjwa. Kutohana na Jiografia ya Wilaya ya Rufiji, huduma za Rufaa zimegawanyika katika Kanda za Kibiti, Mloka na Muhoro. Kanda ya Kibiti inayohusisha maeneo ya Nyamisati na *Delta* ya Kaskazini, inahudumiwa na Gari la Wagonjwa lilioko katika Kituo cha Afya cha Kibiti; Kanda ya Muhoro inahudumiwa na gari lilioko katika Hospitali ya Wilaya ya Itete; na Kanda ya Mloka inahudumiwa na gari lilioko katika Kituo cha Afya cha Nyaminywilli.

**SPIKA:** Ahsante; na sisi tulitumia gari hilo kum-ferry Mheshimiwa Clara kutoka huko mpaka Dar es Salaam.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kulingana na malalamiko ya Wananchi wa eneo la Muhoro; na kwa kuwa ahadi ni deni:-

(a) Je, uamuzi huu wa Wilaya ya Rufiji kupeleka gari Kibiti Serikali haioni kwamba ni kinyume cha ahadi ya Mheshimiwa Rais?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kulipeleka gari hilo Muhoro ambako Mheshimiwa Rais alitoa ahadi na kwa kuwa kuna changamoto ya maeneo ya *Delta* wanakotegema Kituo hicho cha Afya? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sisi hatubishani hapa na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais alielekeza kwamba tupeleke gari Rufiji; hatupeleki gari kwenye Kituo cha Afya tunapeleka kwenye *Planning Unit*, yaani Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, mkishalifikisha pale Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inachukua gari lile inalipeleka Muhoro au inalipeleka katika eneo lingine.

Maelekezo ni kwamba, tunapeleka katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Sasa mimi ananiambia nilizungumza na Mkurugenzi, nimezungumza naye nikamwambia gari lile liliopoombwa kwa Mheshimiwa Rais liliombwa kwa ajili ya Muhoro ndipo akanieleza habari ya Kanda hizo tatu ambazo nimezisema hapa. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anafikiri kwamba bado Muhoro inahitaji, mimi ninasema hapa mwezi wa nne tumepeleka gari jipya na bahati nzuri Mheshimiwa Spika na wewe umesema mlipanda gari hilo. Mimi nitakwenda kufanya hivyo kama anavyoelekeza Mheshimiwa Mbunge, lakini wanao-*plan* kwamba gari liende wapi ni Halmashauri ya Wilaya ya Muhoro.

Kwa kuwa kuna maelekezo ya kupeleka gari pale, jana nimewambia Mkurugenzi Mtendaji kwamba gari hili liliombwa kwa ajili ya Muhoro, kwa hiyo, nitakwenda kufanya kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema. Ninataka kusema hapa ahadi ya Rais ya kupeleka gari Wilaya ya Rufiji imeteketezwa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ninaomba tuendelee na swali la Mheshimiwa Idd Azzan.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa swali hili namba tatu lilihajibowi na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa maswali ya papo kwa papo na kwa kuwa Serikali tayari imeshaanza kuchukua hatua, ninaomba kuliondoa swali hili.

Na. 3

**Agizo la Mheshimiwa Rais Kusitisha Ujenzi – Jangwani**

**MHE. IDD M. AZZAN** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliwahi kuagiza kuwa ujenzi unaoendelea katika maeneo ya Jangwani usitishwe mara moja na eneo hilo libaki kuwa eneo la michezo:-

- (a) Je, ni kwa nini agizo la Mheshimiwa Rais halijatekelezwa hadi leo?
- (b) Je, ni lini agizo hilo litatekelezwa?
- (c) Je, ni hatua gani za kinidhamu zilizochukuliwa kwa waliota kibali cha ujenzi kwenye eneo la michezo?

*(Swali lillilotajwa hapo juu liliondolewa na mwullza swali)*

Na. 4

#### **Tofauti ya Elimu kwa Wananchi**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI** aliuliza:-

Je, Serikali imejiandaaje kuondoa tofauti zilizopo kielimu baina ya wenye uwezo na wasio na uwezo, kijinsia na baina ya maeneo yaliyoendelea sana na yenye maendeleo duni?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imekuwa ikitekeleza suala la utoaji wa elimu kwa usawa kupitia Sera yake ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, ambayo sasa ipo kwenye mchakato wa kuhuishwa hivi punde. Katika kuhakikisha usawa huo, imeanzishwa Mipango ya Maendeleo ya Shule za Msingi (MMEM I na II) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES).

Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) pamoja na malengo mengine, unahakikisha kuwa wanafunzi wote wenye umri wa kuanza shule kwa jinsia zote wakiwemo wenye mahitaji maalum, wenye ulemavu na walio kwenye mazingira magumu kama ya wafugaji na wavuvi, wanaandikishwa wanahudhuria na wanahitimu shule na wale wanaofaulu wanachaguliwa kujunga na Elimu ya Sekondari bila kujali Ukanda fulani, eneo, wala wenye nacho na wasio nacho.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Msingi na Sekondari ni wa Kitaifa, hivyo imewezesha Shule za Msingi na Sekondari kujengwa nchi nzima bila kujali eneo, ukanda, wilaya na kadhalika. Kupitia mipango hii, Serikali imehakikisha kuwa watoto wote wameandikishwa bila kujali maeneo wanayotoka. Aidha, Shule za Sekondari zimejengwa angalau moja kila Kata ili kuwawezesha watoto wote kupata nafasi ya Elimu ya Sekondari karibu na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeupa kipaumbele uwiano wa kijinsia, ambapo unaandikishwa katika Shule za Msingi na Sekondari. Uwiano huu umekuwa wa sawa kwa Wasichana kwa Wavulana 1:1. Aidha, katika Vyuo vya Elimu ya Juu uwiano wa kijinsia unazingatiwa, ambapo Programu Mahsusizi zimeandalialiwa ili kuwasaidia Wanafunzi Wasichana kupata nafasi za masomo hususan katika masomo ya sayansi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa jibu ambalo kwa hakika ninaona halikuzama kwenye tatizo zima nililokuwa ninaliulizia la tofauti baina ya watu wenye uwezo na wasio na uwezo hasa kuhusiana na jinsi watoto wao wanavyopata elimu ni kubwa sana; hili siyo suala tu la kifedha, bali pia ni suala la tofauti baina ya eneo moja na lingine. Sisi ambaa tumetoka kwenye maeneo ambayo hayajaendelea au yalisahaulika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unaelekea kuhutubia ninaomba uulize swal.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Ndiyo nitauliza. Zipo shule nyingi sana ambazo miundombinu yake ni mibovu sana katika maeneo ambayo hayaajendelea; hakuna nyumba za walimu, hakuna maabara na pia walimu wengi hawapo. Je, Serikali imejiendaaje kutatua tatizo hili kwa sababu mipango ambayo imefanywa na Serikali mpaka sasa haijalitatu?

Mheshimiwa Spika, ninaishia hapo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi na kama alivyobainisha Mheshimiwa Kulikoyela, maeneo ya walionacho na wasionacho, ninataka kusema kwamba, Serikali haitambui hilo; Serikali inachojua ni kwamba nchi hii ni moja, inathamini makabila yote, inathamini Kanda zote na watu wote ni sawa; na kama nilivyosema kwamba mipango hii miwili ya MMEM na MMES, imepeleka huduma za shule sehemu zote katika Tanzania, Mikoa yote na hizo shule ambazo anasema kwamba miundombinu ni mibovu, tunakiri baadhi ya shule ni kweli.

Kama nilivyosema ni kwamba, shule zetu kama tulivyokuwa tumezianza mwaka 2006, tunaendelea kukamilisha vitabu, tumeshaanza kupeleka maabara kama nilivyosema wakati wa bajeti kwamba tutajenga vyumba vya maabara na vyombo tumeshaanza kupeleka vile vingunge na mwaka huu tutaajiri walimu wengi sana, mwaka jana tumeajiri walimu 9,200, mwaka huu tutaajiri walimu zaidi ya 25,000 watakwenda huko. Kwa hiyo, ninataka nimtoe wasiwasi kwamba, mambo haya hayajali usawa wa namna anavyoweza kuelewa yeye.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, tunachotaka Mheshimiwa Naibu Waziri ni kujua kwa sababu hata kama mnaajiri walimu wengi, wengi wanaishia mijini; sasa mna programu gani ya *incentives* ambazo kama Taifa tutakuwa tunazijua kwamba walimu wakipangija vijijini wanaweza kwenda kule; mna programu gani ya kuweka vivutio; ndiyo tunataka kujua hilo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Huyu Mheshimiwa Mkosamali amemaliza Chuo Kikuu mwaka huu, mpeni hongera. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri, ninaomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Tuna *incentive* kamili kuhakikisha maeneo yale ambayo yana changamoto kuu kwa walimu kusomesha, kuanzia mwaka huu wa masomo tumeepanga kwamba tutakuwa na fedha za kujikumu katika mazingira magumu jumla ya shilingi 500,000 mara tu walimu wanapokwenda katika shule zile. Chini ya *SEDP II* pia tumeshaanza mkakati wa ujenzi wa nyumba za walimu na tukianzia katika maeneo yale magumu ili kuwe na nyumba ambazo walimu wetu wataweza kufikia na tunaendelea kuhakikisha kwamba, tunaweka miundombinu ambayo itawawezesha walimu hawa kuweza kufanya kazi nzuri katika maeneo haya.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa elimu haina mwisho; na kwa kuwa kuna baadhi ya waajiri huwakatalia wafanyakazi wao kujiedeleza kimasomo mpaka kufikia Vyuo Vikuu kwa visingizio mbalimbali; je, Serikali inasema nini kuhusiano na hilo? (*Makofii*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, tunaineni elimu zaidi, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwasih i wajiri wote wahakikisha kwamba, wanawapa nafasi wafanyakazi wao kwenda kujiedeleza kimasomo. Kwa upande wa walimu, ninawatahadharisha kwamba, wale wanaomala masomo, tutataka kwanza watumikie katika nafasi zao kabla ya kuendelea na masomo ya ngazi nyingine ili wanafunzi hawa wapate nafasi pia ya kufaidika na matunda ya wao kwenda shuleni. (*Makofii*)

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali inafahamu kama zipo baadhi ya Shule za Taasisi za Kidini kama Shule ya Al-Muntazir ya Kishia ina ubaguzi wa Kimadhehebu kama ni kigezo namba moja kwamba ni kigezo cha kufaulu kwa wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ingependa kujua hizo Shule za Taasisi za Kidini ambazo zinafanya ubaguzi katika nchi hii, tuweze kupata taarifa ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Na. 5

**Ukusanyaji wa Mikopo Waliyopewa Wanafunzi**

**MHE. MUNDE ABDALLAH TAMBWE (K.n.y. MHE. SARA MSAFIRI ALLY)** aliliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukusanya madeni kwa wahitimu walioko kwenye ajira rasmi na zisizo rasmi?

(b) Je, Serikali inadai kiasi gani cha fedha zilizokopeshwa tangu kuanza kwa programu hii hadi hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Serikali imeweka mikakati mbalimbali kwa minajili ya kukusanya madeni ya mikopo iliyotolewa kwa wahitimu mbalimbali. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

- (i) Kuidhinisha kupitiwa upya kwa Muundo wa Bodi ya Mikopo na kuongeza nafasi za Watendaji katika Idara ya Urejeshwaji Mikopo. Kwa mwaka 2011/2012, Bodi itaa jiri wafanyakazi wapya 12 katika Idara ya Urejeshwaji Mikopo.
  - (ii) Bodi itaimarisha huduma za kukusanya mikopo kwa kutumia Wakala wa Ukusanyaji wa Mikopo.
  - (iii) Sheria ya Bodi itarekebishwa kuiwezesha kupata taarifa za waajiri na waajiriwa pamoja na wafanyakazi kutoka kwa wadau muhimu kama Mifuko ya Pesheni na TRA.
  - (iv) Bodi itaimarisha elimu kwa umma kuhusu urejeshwaji mikopo.
  - (v) Bodi itawachukulia hatua za kisheria wadau ambao hawatimizi wajibu wao kikamilifu.
  - (vi) Serikali inakamilisha mchakato wa kutoa vitambulisho vya uraia ambavyo vitafanya kazi ya kuwatambua wanufaika wa mikopo mahali walipo na hatimaye kazi ya kurejesha mikopo kuwa nyepesi.
- (b) Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 811.3 zimekopeshwa kwa wanafunzi toka mwaka 1994. Kati ya hizo; shilingi bilioni 106.3 tu zipo tayari kuanza kurejeshwa kutoka kwa wanafunzi 69,143, ambao wamehitimu masomo yao na muda wa matazamio (*Grace Period*) tayari umeshapita.

**MHE. MUNDE ABDALLAH TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wetu wengi wanategemea mikopo ili waweze kuijendeze na elimu ya Vyuo Vikuu; na kwa kuwa kuna uzoroteshwaji mkubwa wa urejeshwaji wa mikopo hiyo; je, Serikali haioni umuhimu sasa wa

kuanzisha Vitengo vya Mikopo katika kila Benki kwa sababu mabenki yote ni wazoefu ili wasimamie ukopeshaji na urejeshaji wa mikopo hiyo na vyeti vya wanafunzi hao vibakie kama dhamana ili waweze kurejesha mikopo na Watanzania wengine wanaostahili waweze kupata? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuanzisha Vitengo kwenye benki kwa ajili ya kukusanya hizi fedha, ilipokuwa inaanishwa Sheria ya Mfuko wa Bodi ya Mikopo, haikuwa imeainishwa hivyo, ninadhani baada ya kuona kwamba kutakuwa na *interest* kubwa na kutakuwa na gharama kubwa na wote tukijua kwamba wale wanafunzi wanapokopeshwa huwa hakuna *interest* na kuna *grace period* ya *ten years* mpaka kurudisha.

Vilevile Bodi ya Mikopo imeweka Wakala wa kukusanya fedha hizo; kuna *Mbinga Auction Mart; Nakala Auction Mart; Microfine Company Limited; Dodoma Universal Trading Company; na Msolopa Investment Company Limited.* Hawa ndiyo wanaokusanya fedha za wanafunzi wanaokuwa taraji wamehitimu na wanatakiwa kurejesha.

**MHE. JOSEPH ROMAN SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kuna tetesi kwamba vijana wengi waliosoma shule binafsi wamekosa mikopo mwaka huu kama kigezo; je, taarifa hizi ni sahihi? (Makofi)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, vigezo vya kuwapatia mikopo wanafunzi wa Kitanzania mwaka huu wa masomo, zimebadilika baada ya Kamati ya Rais, kufanya kazi ya kuchambua mfumo mzuri ambao utawezesha kutoa mikopo. Kigezo kikubwa kilichotumika ni uhitaji; kwa hiyo, mikopo imetolewa zaidi kwa wanafunzi wenye uhitaji kwa maana ya uwezo mdogo na namna ya kuwatambua.

Bodi imetumia njia rahisi ya kuwatambua wale wenye uwezo mdogo, njia ambazo hazina utata wa kuaminika, mojawapo ni historia ya shule ambayo mwanafunzi amesoma; wanafunzi waliosoma katika shule aghali katika nchi yetu, wazazi/ndugu zao wana uwezo wa kuweza kuwashudumia hawakupewa kipaumbele, waliopewa ni wale maskini. (Makofi)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa gharama za Vyuo Vikuu zimekuwa kubwa sana kwa maana ya ada na gharama zingine na kuwafanya wanafunzi wengi kukosa nafasi na uwezo wa kulipia gharama hizo. Kwa kuwa hapa nchini hivi sasa Vyuo Vikuu vya Serikali vimekuwa na gharama kubwa hata kuliko vile vya watu binafsi na kwamba hata hivyo Vyuo vya Serikali vinatoza ada tofauti kwa kila shule. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha *UDOM* kinatoza *degree* ya sheria kwa shilingi 950,000 lakini Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kozi hiyo hiyo inatozwa shilingi 1,500,000.

Je, ni lini sasa Serikali itafanya utafiti huu wa kina wa kujua uhalali wa gharama ya kumsomesha Mtanzania ili gharama hizi zinazotozwa ziwe ndogo kiasi kwamba wananchi wetu wengi waweze kumudu gharama hizo? (Makofi)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO NA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imelibaini hilo na imelitambua kwamba ni tatizo na katika juhudzi za Serikali taraji kwa kushirikiana na Benki ya Dunia tumetoa katika mchakato wa kumpata Mtalaam Mshauri ambaye atatambua/atabaini *students unit cost* ama gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi katika Chuo Kikuu kwa *program mbalimbali*, mara tutakapoweza kupata *students unit cost* na mtaalam huyu tunategemea kumpata mwezi huu wa Novemba, mara tutakapopata hiyo itakuwa ni *basis* ya Serikali ya kuweza kutambua gharama ambazo Serikali ilipe kwa Vyuo lakini vyuo vinaweza vikatozwa kiasi gani kwa wanafunzi wake vile vya Serikali na vile ambavyo siyo vya Serikali.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, atauliza swali hilo. Pia hongera kwa harusi. (Makofi)

## Sera ya Kuzuia Uchanganyaji wa Pamba na Mahindi

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA** aliuliza:-

Sera ya kuzuia uchanganyaji wa Pamba na Mahindi imepitiwa na wakati.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuachana na zio hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inazuia kilimo cha uchanganyaji wa pamba na mahindi kutokana na ushahidi wa utafiti wa kisayansi kuonesha kwamba tija na uzalishaji wa mazao hayo hupungua kwa kiwango kikubwa iwapo pamba na mahindi yatazalishwa kwa kuchanganywa ikilinganishwa na tija na uzalishaji inayopatikana iwapo mazao hayo yatazalishwa bila kuchanganywa. Utafiti uliofanywa katika Wilaya ya Maswa umeonesha kwamba tija katika eneo lililochanganywa ilikuwa kilo 150 za pamba mbegu na gunia mbili za mahindi, wakati tija katika eneo ambalo halijachanganywa ni kilo 800 hadi 1,000 za pamba mbegu na magunia 15 ya mahindi. Tofauti hizo za tija na uzalishaji zinatokana na sababu zifuatazo:-

Kwanza, mazao hayo hushindana kupata mwanga hali ambayo inapunguza ukuaji na uzalishaji kwa kiwango kikubwa;

Pili, kuongezeka kwa mashambuliza ya visumbufu vya mazao hususan wadudu waharibifu kwa kuwa baadhi ya wadudu wanaoshambulia pamba ndio hao hao wanaoshambulia zao la mahindi. Uchanganyaji wa mazao hayo unasababisha ongezeko kubwa la wadudu hao na mashambulizi yao; na

Tatu, uchanganyaji husababisha idadi ya mimea kwa eneo kupungua kwa kila zao na hivyo kusababisha upungufu wa tija na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inazuia uchanganyaji wa mazao hayo vilevile kutokana na sababu ya kulinda afya ya walaji wa zao la mahindi. Hii inatokana na ukweli kwamba udhibiti wa visumbufu vya zao la pamba huhitaji aina tofauti za viuatilifi ambavyo hutumika kwa wingi zaidi na haviruhusiwi kutumika katika zao la mahindi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, nawaasa wakulima wote wa pamba wazingatie ushauri wa kitalaam na kanuni za sheria zinazosimamia uzalishaji wa zao hilo nchini. Kuchanganya mazao hayo mawili kunapunguza tija, uzalishaji na vilevile kunahatarisha afya ya walaji na mazingira kwa ujumla. Nawashauri viongozi katika ngazi zote tushirikiane kuwaelimisha wakulima na wananchi kwa ujumla kuhusu suala hilli.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa majibu ya Serikali yanatofautiana sana na hali halisi ya Wilaya ya Meatu na hasa katika Kata ya Mwanjolo, Mwanyahina, Mwamishale, Nkovoko, Nkoma, Imalaseko pamoja na Mwabuzo ambapo kumeonyesha kwamba hali ya mazao kwa kuchanganya inaridhisha. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuongeza *sample size* ya utafiti ili iweze ku-extend mpaka Meatu ili nao angalau waweze kuruhusiwa ili utafiti uweze kufanikiwa zaidi?

Kwa kuwa utafiti unaofanywa Maswa unaendeshwa na Kituo cha UKiriguru na umeanza mwaka jana na ni utafiti wa miaka mitatu, je, ni kwa nini sasa Serikali inatoa tamko leo kwamba utafiti wa kisayansi umeshafanyika na umeshakamilika wakati ni fedha za Serikali zimekuwa committed, utafiti haujakamilika na Serikali inatoa tamko kwamba tayari utafiti umeshakamilika? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na utafiti siku zote ni suala endelevu. Utafiti hauishii tu mara moja ukasema nimeshamaliza kwa sababu matatizo yanajitokeza kila wakati ndio maana tunaendelea na utafiti. Lakini ninachotaka kusema na kumhakikishia Opulukwa, ni kwamba utafiti kweli umefanyika na hata bila utafiti ukiangalia tu zao la pamba ni fupi, mahindi ni marefu na pamba inataka mwanga, mahindi yapo juu kwa vyovoyote vile haya mazao hayawesi yakashindaniwa mwanga ule, lazima zao moja limshinde mwenzake. Hizi tija tulizoweka hapa ni tija ambazo zimeonekana kabisa baada ya watafiti kufanya utafiti.

Kwa hiyo, mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utafiti wetu uko sahihi lakini bado tunaendelea kufanya utafiti maana utafiti ni jambo ambalo ni endelevu. Sasa endapo kweli katika maeneo haya anayosema Mheshimiwa Opulukwa, wana *data* zingine ambazo zitatuthibitishia kwamba utafiti wetu si sahihi basi nao tutauchunguza. Lakini mpaka sasa hivi utafiti wetu wa kitalaam umetuonyesha hivyo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ni majibu ya kitalaam, tunaendelea na swali linalofuata.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, swali la pili halijabibiwa. Nimeuliza maswali mawili.

**SPIKA:** Okay! Mheshimiwa Waziri jibu swali la pili.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, mimi nadhani Mheshimiwa Opulukwa labda hakunisikiliza, unajua maswali yale yanafanana yote kwa pamoja. Labda niongeze tu kwamba Mheshimiwa Opulukwa, nikuombe kwa sababu suala hili ni la kitaalam zaidi hebu tupate muda mimi na wewe tuweze kulizungumza kwa faida ya wakulima wale. (*Makofii*)

Na. 7

#### **Mkoa wa Singida Kupewa Vocha za Pembejeo za Kutosha Mazao Yote**

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU (K.n.y. MHE. SALOME D. MWAMBU)** aliuliza:-

Mkoa wa Singida hususan Wilaya ya Iramba Mashariki ilipewa vocha chache za majaribio tu na kwa zao la mtama pekee wakati mazao kama mahindi na alizeti nayo yanastawi vizuri:-

(a) Je, Mkoa wa Singida utaondolewa lini kwenye majaribio na kupatiwa vocha za kutosha kwa mazao yote?

(b) Je, ni lini Serikali itatambua kuwa mazao mengine kama mahindi na alizeti yanastawi vizuri na yanastahili pembejeo pia?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida kama ilivyo kwa mikoa mingine unashirikishwa moja kwa moja katika mpango wa ruzuku katika mbolea na mbegu bora za mazao ya chakula hususan mahindi na mpunga kwa kutumia utaratibu wa vocha. Aidha, ruzuku pia hutolewa nje ya utaratibu wa vocha kwa mbegu za alizeti na mtama. Hata hivyo takwimu zinaonesha kwamba matumizi ya pembejeo katika Mkoa wa Singida bado yapo chini sana. Kwa mfano, katika msimu wa mwaka 2010/2011, Mkoa ulipokea vocha zenye thamani ya shilingi 1,725,245,000 na kutumia vocha zenye thamani ya shilingi 1,465,344,500 sawa na asilimia 85 ya thamani ya mapokezi asilimia 15 zilirudishwa.

Katika msimu huo pembejeo zilizopelekwa Mkoani Singida ni tani 2573.10 za mbolea, tani 200 za mbegu ya mahindi na tani 85.97 za mbegu ya mpunga. Aidha, Mkoaa ulipokea tani kumi za mbegu ya alizeti yenyeye ruzuku. Katika mwaka 2011/2012 Mkoaa wa Singida umetengewa tani 2573.10 za mbolea, tani 220 za mbegu ya mahindi, tani 37.31 za mbegu ya mpunga kwa utaratibu wa vocha. Aidha, nje ya utaratibu wa vocha, Mkoaa huo pia utapata tani 20 za mbegu ya alizeti na tani 40 za mtama zenye ruzuku.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini niseme kwamba Mkoaa wa Singida na hususan Wilaya ya Iramba inapata mvua za msimu mmoja tu wa kilimo. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba vocha za pembejeo zikichelewa kufika zikawafikia wakulima kwenye mwezi wa pili hazitatumika, zitaweza kurudishwa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuwaagiza watalaam wake wazifikeshe hizi vocha zilizotengwa kwa wakati na je, anaweza akasema ni lini hizo vocha zitawafikia za mwaka huu kwa sababu tayari wakulima wanazisubiri ili waweze kuzitumia kwa mvua za mwanzo hizi ambazo tayari zimeshaanza Wilayani Iramba? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na matatizo ya ucheleweshaji wa vocha kuwafikia wakulima na hatimaye tatizo linalojitokeza ni mbolea kufika wakati wamekwishapanda. Tumejitalihidi sisi kama Serikali zamu hii kuhakikisha kwamba vocha zile ziwafikie wakulima. Hata hivyo lazima nikiri kwamba hadi ninavyozungumza sasa kuna ucheleweshaji wa vocha hizo. Lakini sheria imechukua hatua, tumechukua hatua kwamba wakati vocha hizo hazijasambazwa siyo Singida tu, lakini katika Mikoa yote ya Tanzania tumepeleka utaratibu wa hati za kupokea mbolea, utaratibu huu umesambazwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote ya Tanzania Bara na utaratibu huo ndio utakaotumika wakati vocha zile hazijafika. Halafu vocha zikifika sasa itakuwa kama ni *retrospective approval*. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwigulu nakuhakikishia kwamba tumechukua tahadhari hiyo na tunajitalihidi ili mbolea ile na vocha zile ziweze kutumika kwa wakati kama iliyopangwa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na uchache wa vocha zinazotolewa lakini bado bei ya vocha za pembejeo hususan mbegu na mbolea ni kubwa sana. Je, Serikali huko ndio kutekeleza sera ya Kilimo Kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Silinde, anasema bado bei ni kubwa, je, huko ndio kutekeleza sera ya kilimo kwanza?

Lakini pia Mheshimiwa Silinde hasemi kwamba utaratibu huo umepunguza bei iliyokuwepo maana bei ambayo mkulima angeitumia ni kutumia kuliko hiyo ambayo ndio anaipata sasa kwa kutumia vocha. Sasa utaratibu tunaoufanya ni kwamba tunaendelea kupunguza huo mzigo kwa mkulima ili hatimaye mzigo huo upungue. Hata hivyo Mheshimiwa Silinde, naomba nikufahamishe kwamba Serikali haina mpango wa kutoa vocha au kutoa ruzuku kwa wakulima wote wa Tanzania, hiyo haiwezekani. Tunachokifanya ni kuchagua baadhi ya wakulima ambao tutawajengea uwezo na utaratibu wa kutumia mbolea ili hatimaye wakijenga uwezo wao wenyewe waweze kuendelea kuinunua mbolea. Kwa mfano, mwaka huu sasa tutatoa kwa wakulima 1,800,000, hao siyo Watanzania wote. Kwa hiyo, huu ni utaratibu tu endelevu tunaendelea kupunguza hili tatizo, lakini mimi nadhani tunatekeleza Kilimo Kwanza kwa sababu tunakwenda kwa *trend* hiyo. (*Makofii*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu huu wa vocha umesaidia sana kuongeza uzalishaji wa chakula pale mahali ambapo utaratibu huu umefanyika vizuri kama katika Jimbo la Peramiho, na uzalishaji ule umesababisha wakulima kuwa na mazao mengi na kwa maagizo ya Serikali ya kutokuuza ziada nje ya nchi, wakulima wengi wamebakiwa na mazao ambayo hawajui watayafanyia nini na watayapeleka wapi.

Je, Mheshimiwa Waziri, yupo tayari sasa kutueleza ni nini Serikali imefanya ili kusaidia kuhakikisha tatizo lile la wananchi kubakiwa na mazao yao na kutokujua mahali pa kuyauza linafanyiwa kazi? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze kwa sababu mliitikia wito na mmezalisha vizuri pamoja na matatizo mnayoyapata. Lakini kwa kweli mmetusaidia kwa sababu mmezalisha sana.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka pia niseme kwamba Serikali imekwishalionna hili siyo kwamba Serikali haioni tatio la wakulima kubaki na mahindi, kwanza kama hatua ya kwanza wenyewe mtakumbuka hata Mheshimiwa Rais alikwishaagiza kwamba turuhusu tu sasa yaanze kuuzwa maana yake mwanzo tulikuwa tumezuia, lakini hivi sasa mnaona mahindi tumekwisharuhusu yaanze kuuzwa nje. Lakini labda nimhakikishie Mheshimiwa Mhagama tu kwamba hivi sasa tupo katika kufanya jitihada za kuyanunua hayo mahindi. Tunajitahidi na ndio maana mnaona hata Waziri wa Kilimo, hayupo hapa kwa sababu yupo anafanya taratibu za kuhakikisha kwamba Wakala wetu wa Hifadhi ya Taifa unapata fedha za kutosha na kuyanunua hayo mahindi ili hayo mahindi angalau tusiwakwaze wakulima wetu.

Naomba wawe wavumilivu kwa sababu Serikali imekwishalionna hili na inalifanyia kazi. (*Makofii*)

Na. 8

#### **Kuzuia Utalii na Uvuvi Haramu Afrika Mashariki**

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR** aliuliza:-

Kenya imekuwa ikifanya utalii na uvuvi haramu katika *Pemba Channel* kwa kutumia nyavu za uvuvi zenye macho madogo zinazoburuzwa na pia utumiaji wa mabomu kadhalika watallii hufika fukwe za Kaskazini Pemba na kufanya shughuli za utalii bila kulipa kodi na kurejea Kenya.

- (a) Je, Serikali inalielewa jambo hili na inachukua hatua gani kuzuia utalii na uvuvi haramu?
- (b) Je, Serikali ipo tayari kuwasilisha tena suala hili kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kupata uamuzi?
- (c) Je, Serikali inajua madhara na athari za vitendo hivi kama vikiachwa kuendelea?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini, lenye vipengele (a), (b) na (c) pamoja na marekebisho yake kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii na uvuvi haramu yamekuwapo matatizo katika maeneo ya Bahari ya Hindi hasa maeneo ya Tanga na Pemba. Uchunguzi uliofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hivi karibuni ulibaini kwamba wavuvi na siyo kutoka Kenya tu pekee yake bali kutoka Tanzania walikuwa wakutumia baruti kuvua na hivyo kuharibu miamba na hazina ya samaki wachanga.

(b) Mheshimiwa Spika, kabla ya kufikisha suala hili kwenye Jumuiya, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zilichukuliwa hatua zifuatazo:-

(i) Kuongeza doria za baharini kwa kutumia vikosi vyta jeshi vya Wanamaji cha Jeshi na vilevile kutumia Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo cha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambapo kwa sasa suala la uvuvi haramu wa kutumia baruti na mabomu limedhibitiwa na limezungu kwa kiasi kikubwa sana;

(ii) Lakini pia hamasa na taratibu nyingi zimetumika katika kuongeza elimu kwa umma juu ya athari zinazotokana na uvuvi haramu wa kutumia baruti na ule wa kutumia nyavu zenye macho madogo za kuburuza. Aidha, kuhusu utalii zipo taratibu zilizowekwa na Serikali zetu hizi, Serikali ya Kenya na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ajili ya watalii kutoka Kenya namna gani watafika katika nchi yetu ya Tanzania na kwa njia gani, taratibu hizo kwa kiasi kikubwa zinafuatwa. Utaratibu wa kuyafikisha masuala kwenye Jumuiya ni wa kawaida na hata kwa masuala haya ya utalii na uvuvi kwa kweli tunashirikiana na Serikali ya Kenya ili kuleta utulivu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu vema juu ya madhara ya kuachia uvuvi haramu na hata utalii usiofuta utaratibu na ndiyo maana Serikali imeendelea kuchukua hatua nilizozieleza juu. (*Makofii*)

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Spika, nina masuala mawili madogo. La kwanza ni kwamba kutokana na watalii wengi kutoka Kenya wanaingia katika Pwani ya Kaskazini ya Kisiwa cha Pemba kwa michezo ya baharini na kwa utalii. Je, Waziri haoni umuhimu wa kuishauri Serikali kuanzisha Kituo cha Uhamiaji Kaskazini Pemba?

La pili, kuna miradi mingi ambayo Jumuiya ya Afrika Mashariki inaisaidia Tanzania. Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ni miradi mingapi ambayo inatekelezwa Zanzibar na kwa kiasi gani imefikia? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, suala la kwanza hivi majuzi tu Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki aliniagiza niende nchini Kenya, nikaenda Mombasa kwa ajili ya kuhakiki usafiri, wavuvi, abiria na watalii baina ya sehemu mbili za Kaskazini Pemba na pale Kenya, Mombasa. Ni kweli kupitia Kamati ya Afrika Mashariki inayoitwa *East African Inter State Security* iliamuliwa kujengwe vituo vya uhamiaji baina ya Kaskazini Pemba na pale Shimoni. Wenzetu Kenya wameshajenga Kituo hicho pale Shimoni na wametii agizo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ningependa kumueleza Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar kwamba hata kule Pemba Kaskazini kipo Kituo cha Uhamiaji pale Wete na kinachajihishwa kwamba kituo hicho kitumike badala ya kupitia njia za panya na kuelekea kule Kenya hasa kwenye njia ya Shimoni.

Lakini swalii la pili, hili ni swalii kwa kweli ni jipya kabisa. Lakini kwa faida ya Watanzania na hasa wale walipo Zanzibar na kwa ruhusa ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kueleza tu kwamba kuna miradi kama minne hivi ambayo hivi sasa inashughulikiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kwanza ni mradi wa kutengeneza njia za feri, uwiano wa feri kutoka Mombasa - Tanga, Pemba - Zanzibar, Dar es Salaam na Mtwara. Mradi wa pili ni wa ujenzi wa Bandari ya Maruhubi na mradi wa tatu ni mradi wa kuongeza thamani mazao ya kilimo ambayo yanazalishwa pale Zanzibar. Mradi wa nne ambaa hivi sasa umefikia katika hatua kubwa sana ni mradi wa kutengeneza kiwanja cha ndege pale Pemba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi huu sasa hivi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa hivi sasa mradi huu upo katika hatua ya ufadhili kupitia ADB katika hatua za mwisho kabisa. Kwa hayo, machache naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

Na. 9

#### Saratani ya Kongosho Dume

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Je, Serikali inafanya juhudii gani za kuwafanya uchunguzi wanaume wenye umri mkubwa ili kubaini kama wamepata ugonjwa wa Saratani ya Kongosho Dume ili wapatiwe matibabu

mapema kama wanavyofanya kwa kikundi cha MEWATA kwa kufanya uchunguzi wa Saratani ya Matiti na Shingo ya Uzazi kwa wanawake?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza sana waanzilishi na wahanga wa ugonjwa wa Saratani ya Kongosho Dume Mchungaji Canon na Dokta Emmanuel J. Kandusi kwa kuanzisha kampeni ya ugonjwa wa Saratasi, pia Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) kwa kazi nzuri wanayoifanya kuisaidia Serikali kupambana na maradhi ya Saratani nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi a Jamii imeanzisha kitengo cha kushughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza (*Non Communicable Diseases*) ikiwemo Saratasi ya Kongosho Dume jina la Kiingereza (*Prostate Cancer*). Moja ya kazi ya kitengo hicho ni kutoa elimu ya afya kuhusu kujikinga na visababisha vya maradhi ya Saratani na kubadilisha tabia inayochangia kupata ugonjwa wa Saratani ikiwemo Kongosho Dume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma hiyo, Serikali inakusudia kuwapa elimu watoa huduma wote wa afya katika ngazi ya Wilaya ili waweze kuwafanyia uchunguzi wa tezi dume wanaume wenye umri kuanzia miaka 50 na kugundua mapema tatizo hili, ili wawape rufaa kwenye hospitali yenye uwezo wa kuwapatia matibabu.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Afya nataka kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa katika jawabu lake Mheshimiwa Waziri amesema Serikali inakusudia kuwapa elimu wataalam wa afya katika ngazi ya Wilaya, kukusudia na kutenda ni mambo mawili tofauti. Hata binadamu kwa kawaida wanaweza kukusudia kuo katika miaka mia wala hajaoa. Je, Serikali ina mikakati gani ya dhati na ni mwaka gani wataanzisha vitengo vya kuwapa huduma ya kuwagundua watu wenye maradhi haya hasa ukizingatia kwamba maradhi haya yanazidi kukua siku baada ya siku?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, maradhi haya ni gharama na Mheshimiwa Waziri kutokana na jawabu lake analotoa hapa kwamba baada ya kugundulika kwamba wenye maradhi haya watapatiwa ufumbuzi wa kupelekewa au kupewa rufaa kwenda hospitali nyingine, je, Serikali ipo tayari sasa kubeba gharama za walalahoi hawa walipo Wilayani ambao watapata kwenda katika hospitali moja kati ya hospitali tatu ama hospitali ya Moshi, *Ocean Road* au hospitali iliyopo Bugando? Ahsante.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, (a) au moja, suala la kukusudia kuwapa elimu watendaji katika ngazi ya Wilaya. Wizara yangu imejipanga na tunatengeneza sasa hivi mikakati ambayo tutaingiza katika Bajeti ijayo kuanza kutekeleza mkakati huu kwa vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ameelezea kuwa anataka kujua nani atabeba hizi gharama za matibabu kwa hawa wananchi wenye kipato cha chini, tutawasaidiae? Naomba ifahamike kwamba matibabu ya Kansa kwa sera yetu na utaratibu kwamba yanatolewa bure, iwapo kwamba wananchi wanatozwa hela kwa sababu pengine hizo dawa hazipo kwa muda ule lakini dhamira yetu na mikakati yetu na sera kwamba matibabu haya yawe bure na tumedhamiria hivyo na tutazidi kuboresha mwaka hadi mwaka hadi tufikie siku moja wananchi kule wanapata huduma hizo za bure.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Swali langu la nyongeza kwa kiasi fulani limejibiwa na Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulize swali dogo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla matibabu ya Saratani ni ghali sana na wananchi wengi wanashindwa kumudu, je, ni lini sasa Serikali itatoa matibabu ya Saratani ya aina zote bure kama ambavyo inafanya kwa magonjwa ya walioathirika na UKIMWI? Ahsante sana.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, matibabu ya ugonjwa wa Saratani tumedhamiria hasa kuwalenga wale ambao hawana uwezo kabisa na matibabu haya yatatolewa bure. Kama jibu langu la kwanza katika swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Sanya nimefafanua zaidi kwamba tutaliingiza katika Bajeti ijayo ya fedha mwakani, hili litaonekana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, kabla sijajibiwa swali naomba kujua kwamba hii *microphone* yangu itatengenezwa lini, ni mwaka mzima haijawahi kufanya kazi. (*Kicheko*)

Swali la nyongeza, kwa kuwa Serikali mwaka jana wakati Naibu Waziri akijibu swali kama la mambo ya Saratani alikiri kwamba sababu mojawapo inayosababisha masuala ya kansa ya akinamama kwa shingo ya uzazi, matiti na shingo ya uzazi na kongosho dume ni suala la matumizi ya vyakula na mafuta.

Napenda kujua baada ya Serikali kugundua hilo, ni juhudhi gani zimefanywa kutoa elimu kwa wananchi ili kuweza kuhakikisha kwamba tatizo hili la ongezeko la magonjwa ya kansa linapungua? Ahsante.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, suala la elimu kwa umma Wizara yangu tayari imeshaanza kutoa elimu hiyo na ndani ya Bajeti ya mwaka huu mojawapo ya vitu ambavyo vitapewa kipaumbele ni namna gani tunaweza tukakabiliana na magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo na ugonjwa huu wa Saratani. Kwa hiyo, tunatumia kutoa elimu kwa kutumia redio, televisheni na vyombo vingine. Vilevile tunawatumia wadau wengine ambao nao wanatoa mchango huu katika sekta ya afya. Lakini naomba nimhakikishie tena kwamba bado hii ni programu ya muda mrefu na kama bado haijakufikia hiyo elimu au taarifa au kampeni hiyo ya uelimishaji bado siku zinazosogea hiyo elimu itakufikia.

Na. 10

#### **Uwezo wa Kituo cha Matibabu ya Saratani *Ocean Road***

**MHE. HAMAD ALI HAMAD** aliuliza:-

Ugonjwa wa Saratani huwakumba wananchi wa rika zote na kutoka katika maeneo yote ya nchi yetu. Je, kituo cha matibabu cha ugonjwa wa Saratani cha *Ocean Road* kina uwezo wa kulaza wagonjwa wangapi kwa wakati mmoja?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* ina jumla ya vitanda 120 lakini kutokana na wingi wa wagonjwa Taasisi hiyo hulaza wagonjwa zaidi ya 200 wengi wao wakiwa ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukabiliana na tatizo hili, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imegharamia ujenzi wa jengo jipya kwa ajili ya wodi. Jengo hili litaongeza uwezo wa vitanda 170 litakapokamilika hivyo kutakuwa na jumla ya vitanda 290. Kazi ya ujenzi inaendelea vizuri na ipo katika hatua za ukamilishaji.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Serikali imeamuza kufanya Mji wa Dodoma kuwa Mji Mkuu, hatuoni kwamba kuna haja ya kuanzisha kituo hiki katika hospitali ya Wilaya hapa Dodoma?

Pili, je, ni lini Serikali itapeleka wataalam ili kusaidia kwa upande wa Zanzibar ili kupunguza usumbufu wa kusafiri kufuata huduma hii Tanzania Bara kwa Wazanzibar? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi matibabu haya tunayatoa katika Hospitali za Rufaa na zile hospitali ambazo zipo katika ngazi ya Kanda, Dodoma haipo katika mojawapo ya hizo hospitali. Lakini hata hivyo angalizo hili tumeliona, tutaangalia namna gani kama tutaweza kulipatia ufumbuzi.

Swali lake la pili lini tutapeleka watalaam Zanzibar? Ni dhamira yetu vilevile *ku-support* wenzenetu wa Zanzibar kwa zile taaluma ambazo wao hawana na huduma ambazo hazipo. Lakini kwa sasa hivi tuna utaratibu kwamba bado tunapokea wagonjwa kutoka Zanzibar kwa rufaa kwenye hospitali ambazo zipo Tanzania Bara. Lakini hata hivyo nilipata nafasi kabla sijaja kwenye Bunge hili kuongea na Waziri mwenzangu Mheshimiwa Juma Haji Duni na ye ye akanieleza kwamba wana mikakati nao ya kufanya utaratibu wa kuanzisha huduma hizo kule Zanzibar na sisi tutawaunga mkono. (*Makofi*)

Na. 11

#### **Gereza la Kihesa Mgagao Kuhamishwa**

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA** aliuliza:-

Tarehe 5 Agosti, 2008 Mheshimiwa Rais aliagiza kuwa Gereza la Kihesa Mgagao mahali ambapo palikuwa na Kambi ya Wapigania Uhuru wa Afrika Kusini, Zimbabwe na Namibia lihamishwe ili kulinda historia:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo hilo?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza limeshatekeleza agizo hili, kwanza lilianza kwa kufufua mipaka ya eneo linalomilikiwa na Jeshi la Magereza katika eneo hilo, baada ya kutekeleza zoezi hilo, ikigundulika kuwa wananchi walikuwa wanatumia ekari 335 kwa kilimo na makazi ambazo zipo ndani ya eneo la magereza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza liliamua kuwaachia ekari 335 ambapo tayari walikuwa wanaishi pamoja na eneo lingine lenye ukubwa wa ekari 254 ambazo ndani yake kuna majengo yanayotumika kama Gereza na Makazi ya askari kwa kuzingatia agizo la Mheshimiwa Rais. Kwa ujumla Jeshi la Magereza litawaachia wananchi eneo lenye ukubwa wa ekari 1,228.

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Jeshi la Magereza umeshatoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilolo kwa barua Kumb. Na. HOC.59/F/1/9 ya tarehe 18 Februari, 2011 juu ya hatua hizo. Kinachosubiriwa ni taarifa kutoka kwa mamlaka husika mkoani Iringa ili Jeshi la Magereza liweze kukabidhi eneo hilo kwa wahusika. (*Makofi*)

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nyininge niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza kabisa nasikitika kwamba jibu lilitolewa haliendani na swali, swali lilikuwa Rais aliagiza Jeshi la Magereza lihame kutoka Kambi ya Kihesa Mgagao na wapewe eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, jibu linalotolewa sasa ni kwamba wamezidi kugawana na wananchi ambalo halikuwa agizo. Na mara baada ya agizo lile Halmashauri ya Wilaya ilitafuta maeneo mawili, moja ikiwa ni kijiji cha Lulanzi na nyingine ni kijiji cha Lukani ili wachague mojawapo. Lakini wao kutokana na jibu hilo ni kwamba wanaendelea kutumia pale kama Gereza.

Je, Serikali haioni kwamba kufanya hivyo ni kudhalilisha historia ya wapigania Uhuru waliotoka Afrika ya Kusini, Zimbabwe na Namibia?

La pili, kwa kuwa Kambi za Wapigania Uhuru nyingi hapa nchini sasa hivi zinatumika kwa ajili ya maendeleo ya jamii, mathalani pale Mazimbu Morogoro sasa kinatumika kama Chuo Kikuu na kimeruhusu nafasi kubwa kupanuka pale. Ukienda Wami Dakawa inatumika kama *High School*, ukienda Kongwa inatumika kama *Secondary School*, ukienda Bagamoyo kama *Secondary School*, Nachingwea hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ni nini kinachozua Serikali kuruhusu Kihesa Mgagao itumike kwa maendeleo ya jamii kama inavyotumika mahali kwngine hasa baada ya kupata mfadhili wa kujenga shule ya wasichana kwa eneo hilo? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubali na nakiri kwamba, maneno anayozungumza Mheshimiwa Mbunge, Profesa Msolla, tumeyazungumza katika kipindi cha nyuma na nimshukuru kwamba amekuwa ni mfuatiliaji mzuri kwa suala hili. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jibu lilitolewa ndio hasa jibu ambalo linastahiki kwa swali alilouliza kwa sababu, maeneo mengine ambayo ameyataja Profesa Msolla, nakubaliana na yeye kwamba, kambi zilipoachwa na wakimbizi na kurejea katika nchi zao pale uamuui ulichukuliwa na hatua zikachukuliwa kufungua shule, kufungua vitu vingine na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili eneo la Kihesa Mgagao, ilitambulika kweli kwamba kuna historia pale, zilikuwa ni kambi za wapigania uhuru wa nchi ambazo amezitaja za Namibia, Zimbabwe, Afrika Kusini na kadhalika. Lakini tatizo ni kwamba, wakati walipotoka hawa gereza tayari liliuwepo pale, tatizo ambalo tumekuwanalo sio kwamba tunakiuka ama tunakwenda kinyume na agizo la Mheshimiwa Rais, kitu ambacho hakiwezi kikafanyika kwa sababu mbali ya kwamba huyu ni Rais, lakini huyu ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kinachozungumzwa hapa ni kwamba, tuko katika hatua za utekelezaji. Iwapo tunafunga hili gereza ni lazima liwepo gereza lingine na hizo ndizo hatua ambazo tunazichukua kwa maana ya kusema kwamba, tunapata eneo na eneo karibu lote tutawaachia ili tuweze kwenda katika historia ambayo ni kubwa, Tanzania imeweka mchango wake katika *liberation* ya hizi nchi za Kiafrika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kujibu swal lake la pili niseme tu kwamba, hakuna kigugumizi wala hakuna kitu chochote ambacho kinatufanya sisi tusite, isipokuwa tatizo ni kwamba, kuna wafungwa ambao wapo katika gereza hili. Sasa ni suala tu la kupata eneo lingine na mchakato kweli unaendelea na tumeshapata eneo lingine. Ni suala tu la utekelezaji kati ya gereza na Serikali ya Mkoa wa Iringa, viongozi pale kuweza kupata suluhu katika hili. Nimhakikishie Profesa Msolla kwamba, tunafuatilia kwa makini na hili litatmia.

**SPIKA:** Mwende mkaliongee huko huko vizuri zaidi. Bahati nzuri hakuna kinachofanana na gereza hili kwa hiyo, swal lingine halipo. Mheshimiwa John Paul Lwanji, aulize swal linalofuata.

Na. 12

#### Njia ya Itigi – Tabora Kuwekewa Vituo vya Polisi na Gari la Doria

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Njia ya reli na barabara kutoka Itigi – Tabora, inayopitia maeneo ya Kitaraka, kazikazi, Chaya, Kalangasi, Tura, Malongwe, Nyahau, Goweko, Igulula, Itulu na Kigwa, ina mapori makubwa ambayo majambazi hufanya uhalifu mara kwa mara:-

- (a) Je, kwa nini kuna Vituo vya Polisi viwili upande wa Tabora na kimoja upande wa Singida?
- (b) Je, ni lini vituo vingine vitaanzishwa katika maeneo yaliyotajwa?
- (c) Je, ni lini Serikali itatoa gari la doria katika Kituo cha Itigi ili kupambana na uhalifu katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, katika upande wa Tabora visto vituo viwili na upande wa Singida kipo kituo kimoja cha Itigi. Maeneo mengine yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, hayana vituo vya Polisi kwa sababu ya tatizo la rasilimali fedha. Hata hivyo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida, linajitahidi sana kupunguza uhalifu katika maeneo hayo kwa kushirikiana na askari wanyamapori na wananchi kwa kuitao wa ulinzi shirikishi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga Vituo vya Polisi na nyumba za askari wasiopungua tisa kwa kila Kata au Sheha, nchi nzima yakiwemo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Mpango huu unatekelezwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wananchi na TAMISEMI. Tunayo taarifa kwamba, wananchi wa Kata ya Kitaraka wameshaanza mchakato wa ujenzi wa kituo hicho. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, atusaidie kuwashamasisha wananchi wa maeneo mengine ili washiriki katika mpango huu muhimu.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa kutokana na uhaba wa rasilimali fedha, Serikali haitawenza kukipatia gari Kituo cha Itigi ambacho kinazo pikipiki tatu hivi sasa na pale inapobidi kitahudumiwa na magari yaliyopo Wilayani Manyoni.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mhesimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, tumeambiwa hapa tatizo la rasilimali fedha na kwamba, Polisi wamekuwa wakishirikiana na Idara ya Waqnyamapori. Lakini taarifa niliyonayo ni kwamba, eneo lile lililuhisha Chaya, ambayo ni Mbuga ya Uwindaji kwa kushirikiana kwa pamoja na Mbuga ya Hifadhi ya Muheki Kizigo, huingiza takriban shilingi bilioni 1.9 kwa mwezi, Hazina na eneo hilo ni tajiri na lina rasilimali za kutosha. Je, Serikali haikuona kwamba haikufanya utafiti wa kutosha katika kujibu sehemu ya suala hili?

Mheshimiwa Spika, la pili. Ni kweli kwamba, hutokea magari ya kuja kufanya doria kutoka Manyoni au Singida, lakini hiyo hutokea mara baada ya matukio, lakini kabla ya matukio hakuna gari la aina yoyote na kutoka Itigi mpaka Tabora ni takriban kilometra 300 na vituo hivi ni 12, sasa mpaka litokee tukio ndio wafike. Sasa nadhani kinga ni bora kuliko tiba. Je, bado Serikali haionti kwamba, kuna umuhimu wa kuweka gari katika kituo cha Itigi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, masuala haya Mheshimiwa Mbunge Lwanji, rafiki yangu, tumekuwa tunayazungumza sana na nimejitahidi kadri nilivyowenza kukufahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwa heshima zote kwamba, tunazingatia umuhimu wa kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo katika maeneo husika. Lakini pia kila mara nimekuwa namwambia, endapo rasilimali fedha itaruhusu tutajitahidi kwa kadri tuwezavyo kuhakikisha kwamba tunampatia vitendea kazi kwa wale askari walio katika maeneo haya. Sasa askari wanyamapori ambao tunajaribu kusaidiana nao, hii ni Wizara tofauti na Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini bado tuna ule mtandao wa kushirikiana, ila bado hatujafikia kwenye mtandao wa kushirikiana katika rasilimali fedha, lakini totalitazama hilo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kuhusu swali lake la pili kwamba, ni kweli wakati mwingine tunajitokeza kwa maana ya Polisi baada ya matukio na sio kabla ya matukio. Lakini hii inaendana na hali halisi ambayo tunayo katika Taifa letu, ambayo ni uhaba wa rasilimali fedha, lakini jitihada kwa kweli zimekuwa zinafanyika na sio kwamba hatuoni umuhimu wa kuweka hivi vituo ama kuweza kumpatia gari Mheshimiwa Mbunge, lakini nataka nimwombe, hili ni suala ambalo tutakuwanalo na tutalizingatia na endapo rasilimali fedha itaruhusu, huko mbele ya safari nimhakikishie kwamba, hilo tutaweza kulitimiza.

Na. 13

**Upatikanaji wa Umeme wa Uhakika  
katika Mkoa wa Kigoma**

**MHE. DAVID Z. KAFULILA** aliuliza:-

Kwa muda wa nusu karne sasa Mkoa wa Kigoma unapoteza fursa kubwa za uzalishaji na maendeleo kutokana na kukosa umeme bila sababu za msingi:-

(a) Je, ni lini Mkoa huo utapata umeme wa uhakika ikilinganishwa na mahitaji yake kihuduma na kiuchumi?

(b) Kwa kuwa, ni Sera ya Serikali kuhakikisha umeme unakuwepo katika Makao Makuu ya Wilaya. Je, ni lini Wilaya ya Uvinza itapata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma kuanzia mwezi wa Sita mwaka jana 2010, baada ya ufungaji wa mitambo mipyaa iliyanunuliwa na Serikali ya aina ya ABC, ilipata nyongeza ya kilowati 6,250 juu ya kilowati 3,600 zilizokuwepo kabla ya hapo ambazo ziliikuwa hazitoshelezi mahitaji ya Kigoma, kwa maana ya Kigoma Mjini. Jumla ya kilowati 9,850 zilizopo kwa sasa katika Mkoa mzima zinatosheleza mahitaji ya sasa na kuzidi, kwani mahitaji ya juu kwa sasa ni kama kilowati 5,500.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa kuunganisha umeme kwenye maeneo ya Uvinza, ulikuwa umeainishwa na mradi wa kufua umeme kutoka Mto Malagarasi, ambapo chanzo cha maporomoko ya awali kilihamishwa kutokana na viumbwe adimu ambaao wangeathirika na mradi kama ungetekelawa. Kama ambavyo tulishaeleza hapa Bungeni, mradi wa kufua umeme wa awali ulikuwa ujengwe katika maporomoko ambayo yalipewa jina la Igamba II. Tafiti nyingine imebaini kuwepo kwa maporomoko yanayofaa katika maeneo mbadala ya Igamba III na ripoti ya mradi huo imeshafanyika na kukabidhiwa kwa Serikali kwa ajili ya kujadiliwa na wataalam wa *TANESCO* na kufanyiwa tathmini inayostahili.

Serikali pamoja na Shirika la Umeme la Tanzania (*TANESCO*), inatafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza tena mradi huo katika mazingira hayo mapya na kuzingatia pia vigezo hivyo vyta ulinzi wa mazingira ya kipekee na maslahi mapana ya kijamii.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nasikitika kwa majibu ambayo hayajitoshelezi kwa sababu, nilichouliiza ni lini kwenye mipango ya Serikali, Mkoa wa Kigoma utapata umeme? Sasa jibu la lini hapo halipo! Serikali inatafuta fedha, haisemi fedha ni kiasi gani ambazo zinatakiwa! Kwa hiyo, hili jibu lina upungufu.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la nyongeza ambalo ningependa kuuliza hapa ni kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba, Kigoma Mjini kuna ziada ya umeme; haya majibu

aliyatoa katika kikao kilichopita, lakini tukakubaliana kwamba nyongeza ile au ziada ile ipelekwe Vijiji vya Jimbo la Kigoma Kaskazini na Kusini kwa kuanzia kwa ajili ya kuondoa hiyo tofauti. Ningombwa Mheshimiwa Naibu Waziri, atupatia majibu kwamba mpango huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa kupata majibu ya Serikali, kwa sababu Serikali ni lazima iwe na mipango. Ningependa kupata majibu ni lini kwenye mipango ya Serikali, Kigoma itapata umeme wa uhakika kwa maana ya Igamba III itakamilika pamoja na gharama zake?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie tu Mheshimiwa kwamba, nimejibu swali lake kulingana na aliyoulima. Ameuliza swali la upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Kigoma na ametumia neno umeme wa uhakika. Sasa kitaalam katika upatikanaji wa umeme, umeme una *categories* tatu; una *category* ya *affordability*, una *category* ya *sustainability* na una *category* ya *availability*. Sasa yeche anachozungumzia hapo ni *sustainable availability*. Sasa nimejibu hivi, nimemwambia kwamba, upatikanaji wa umeme Mkoa wa Kigoma, miaka miwili iliyopita Mkoa mzima wa Kigoma, ulikuwa na *megawatt* nne, sasa hivi Kigoma nzima ina *megawatt* karibu 10 na hiyo ni jitihada ya Serikali hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa ukikataa kukiri hilo, labda wewe hukuwepo, lakini Wabunge wa awali wasingeweza kukataa kukiri hilo. Sasa ninachosema ni kwamba, Mkoa wa Kigoma ni Mkoa mpana, kuna mahitaji kuanzia kule juu Kibondo ambayo yamepelekewa jenereta, kule mahitaji yale yatakwendwa mpaka Kakonko kwenye Wilaya mpya. Kuna mahitaji kwa Mheshimiwa Agripina kule Kasulu; mwanzo nilipojibu swali lile nilisema kwamba, tatizo liliikuwa upatikanaji wa vifaa. Sasa hivi umeme umepatikana majenereta yamewashwa, wateja zaidi ya 400 wameomba kuunganishwa na wameunganishiwa wateja 400, lakini kuna wateja wengine 500 Kasulu wameomba kuunganishiwa umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hayo ni majibu ambayo yanakuelekeza kwamba, umeme wa uhakika umepatikana katika maeneo hayo, wa maana ya Kibondo, Kasulu, Kigoma. Sasa unauliza Uvinza, Uvinza ni Wilaya mpya hata *DC* hajateuliwa! Sasa tutakopofika katika hatua hiyo ya kuwa na Wilaya mpya ya Uvinza, kwa sababu Serikali hii ina utaratibu wa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu mapya ya Wilaya zote na Uvinza utakwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imejipanga na kwenye Wilaya mpya ya Uvinza ambayo nadhani mzee ndio Wilaya yake, namhakikishia kwamba, Serikali itapeleka umeme kwa utaratibu wa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote.

**SPIKA:** Tunaendelea, hakuna Wilaya inayofanana na hiyo aliyoulima Kafullila. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya...

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, swali la pili hajalijibu. Kwamba, aliahidi ziada ya umeme itakwenda Vijiji vya Kaskazini vya mwanzoni na Kusini; ndio swali la pili, hajalijibu.

**SPIKA:** Hayo ni mambo ya ndani, mtafanya huko. Ukifika utapatikana, ilimradi mradi wa ziada upo.

Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, aulize swali linalofuata. Yuko wapi? Kwa niaba yake ni nani anauliza?

Haya Mheshimiwa Mtanda, kwa niaba ya Mheshimiwa Innocent.

Na. 14

#### Athari za Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

**MHE. SAID M. MTANDA (K.n.y. MHE. INNOCENT E. KALOGERIS)** aliluliza:-

Vijiji vya Kiburumo, Bwila Juu Kata ya Selembala, Wilaya ya Morogoro Vijijini, vimetajwa na Serikali kuwa vitaathirika na ujenzi wa Bwawa la Kidunda, litakalowezesha Mji wa Dar-es-Salaam, kupata maji ya uhakika tangu mwaka 2008:-

- (a) Je, Serikali ina tamko gani kwa wananchi hao juu ya ujenzi wa bwawa hilo?
- (b) Je, wananchi wangapi toka vijiji gani wataathirika na mradi huo kama upo?
- (c) Je, ni lini tathmini ya mali itafanyika ili wananchi hao wapate haki zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakati wa kuwasilisha Bajeti ya mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Bunge lako Tukufu, ilitoa maelezo kuhusu ujenzi wa bwawa la Kidunda. Katika mwaka huo kazi zitakazofanyika ni pamoja na kufanya tathmini ya mali ili kulipa fidia kwa wananchi watakaobainika kuathiriwa na shughuli za mradi huo na pia, kubaini maeneo yatakayotumika kuwahamishia wananchi baada ya kufidiwa. Vijiji vya Kiburumo na Bwila Juu Kata ya Serembala, Wilaya ya Morogoro Vijijini, ni katika vijiji vinavyotakiwa kuhamishwa kupisha ujenzi wa bwawa hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika utafiti uliofanyika ulionesha kuwa vijiji vinne vitakavyoathirika moja kwa moja na shughuli za mradi ambavyo ni Bwila Juu, Bwila Chini, Kiburumo na Kidunda ambavyo vina jumla ya vitongoji 14 na vinakadiriwa kuwa na Kaya katika ya 561 hadi 600 zenye wakazi wapatao 2,700. Kwa sasa, uchambuzi wa takwimu unafanyika ili kupata idadi kamili ya wakazi, nyumba, mashamba na taasisi kama shule na zahanati.

(c) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Morogoro Vijijini imeanza zoezi la kuthamini mali za wananchi watakaotakiwa kupisha ujenzi wa mradi tarehe 5 Novemba, 2011. Wizara itaanza kulipa fidia baada ya taarifa ya tathmini hiyo kukamilika.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Kalogeris. Je, kwa kuwa, tathmini hii...

**SPIKA:** Hilo ni lako mwenyewe.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa tathmini hii imeanza tarahie 05 Novemba, nataka kujua tu ni lini tathminni hii itakamilika ili wananchi wa maeneo hayo waweze kufahamu hatima yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini ndio inafanya zoezi la kutathmini, nategemea kabisa Mbunge, atashiriki pamoja na wananchi kuweza kufanya zoezi hili liende haraka. Mara zoezi likiwa tayari tutawajulisha ili kusudi waweze kulipwa fidia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, ujenzi wa Bwawa hili la Kidunda lilioko Morogoro ni kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Dar-es-Salaam na kwa kuwa, bwawa hili limesimama kwa muda mrefu toka mwaka 2008 na kwa kuwa, katika bajeti ya mwaka huu ya Serikali, kumetengwa shilingi bilioni sita tu peke yake za kulipa fidia wakati kwenye mpango wa Taifa wa miaka mitano zilipaswa kwenye mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 kutengwa bilioni 26.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ipo tayari kupitia fedha ambazo nafahamu imezipata kwa mkopo kutoka India kwa ajili ya miradi ya maji; iko tayari kuelekeza fedha za ziada ili ujenzi huu

uweze kuanza mwaka huu kwa ajili ya kumaliza tatizo la maji Dar-es-Salaam ikiwemo Jimbo la Ubungo mapema iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mnyika kwamba, fedha zilizotengwa ni kwa kazi ambayo imeratibiwa kufanywa kati ya sasa na Disemba. Sasa hivi Mhandisi Mshauri, anafanya usanifu wa mwisho na baada ya hapo ndio tutaanza kutangaza tenda kwa hiyo, ujenzi wa bwawa hili utaanza mwaka wa fedha kuanzia Januari na kuendelea. Kwa hiyo, fedha za kuanza hilo bwawa zipo. Kwa hiyo, sisi tunaomba asiwe na wasiwasi.

Na. 15

#### **Mradi wa Maji Vijiji vya Ngara**

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Miaka mitatu sasa imepita tangu wananchi wa Vijiji 13 vya Ngara waahidiwe kupelekewa maji chini ya mradi wa Benki ya Dunia na kutakiwa kuchangia shilingi milioni tatu kila Kijiji ambazo walichanga na kuweka benki na hivi sasa zimeshapungua kutokana na makato ya Benki:-

- (a) Je, ni lini Vijiji hivyo vitapatiwa maji chini ya Mradi wa Benki ya Dunia?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufidia makato yaliyofanywa pindi itakapofikia hatua ya utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukumazima, Mbunge wa Ngara lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na washirika mbalimbali wa maendeleo ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia. Utekelezaji wa programu ulianza mwaka 2007/2008 kwa kujenga miradi ya maji yenye kuleta matokeo ya haraka. Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, miradi ilijengwa katika Vijiji vya Runzenze, Buhororo, Kasharazi, Ruganzo, Kumtana, Muyenzi, Kasulo, Bulengo, Mugoma, Shanga, Bugarama, Mumirama, Nyanzari, Nterungwe, Kirushya, Nyakiziba na Kanyinya ambapo miradi yote inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Vijiji 10 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara inatekelezwa katika Vijiji vya Namubuku, Mbuba, Kumbuga, Rulenge, Murugarama, Kanazi, Rwinyana, Mukibogoye, Kabanga, Muhweza, Munjebwe, Muruvyagila na Kabalenzi. Usanifu ulikamilika na mkandarasi wa uchimbaji visima ameajiriwa na ataanza kazi mwezi huu wa Novemba, 2011. Kazi ya kuchimba visima itaanza kwanza katika vijiji vinne vya Mbuba, Rwinyana, Kumbuga na Namukubo. Kijiji cha Rulenge kitatumia teknolojia ya maji ya mtiririko ambapo ujenzi wa miundombinu utaanza mwezi Januari, 2012. Jumla ya shilingi milioni 554 zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Utekelezaji wa miradi katika vijiji vilivyobaki utafanyika kwenye awamu ya pili ya programu itakayoanza mwezi Julai, 2012.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2010 wananchi walikuwa wamechanga jumla ya milioni 21,321,472 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Hata hivyo, kiasi hicho kitakuwa tofauti kutokana na makato ya huduma ya benki na faida, ambapo makato na faida ni suala la kisheria kwa ajili ya utunzaji wa fedha zote zinazokuwa benki. Kwa kuwa wananchi hatawachangia tofauti ya kiasi kitakachopungua kutokana na makato ya benki, suala la fidia halipo.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza, kwanza niishukuru

Serikali kwa kutoa ahadi ya uhakika *firm commitment* kwa wananchi wa Ngara kwamba mkandarasi ameshaajiriwa na ataanza kuchimba visima katika Vijiji vya Mbuba, Rwinyina, Kumbuga na Namukubu. Swali, Serikali ilishawaahidi wananchi wa Ngara kwamba mwaka huu vijiji viwili vya Rulenga na Ngundusi vingeanza kupatiwa maji ya *World Bank*, lakini Kijiji cha Ngundusi hakijitokezi kabisa katika jibu la Mheshimiwa Waziri, naomba anieleze kwa nini ahadi hiyo sasa imebadilika? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, lazima niwapongeze wananchi wa Ngara kwa kuitikia wito wa kuchangia miradi ya maji na wameweza kuchanga. (*Makofii*)

Pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ntukamazina kwamba vile vijiji ambavyo havitawenza kuanza kwa sasa tunasema vitaendelea katika awamu ya pili ambayo inaanza Julai, 2012. Sasa hivi Serikali inaongea na hawa wafadhili, maana ile awamu ya kwanza ilikuwa iishe Juni, 2012. Sasa tunaongea nao tunataka tu-*extend*, mwaka mmoja zaidi ili kusudi vijiji vingi viweze kutangaza miradi na kujenga miundombinu. Kwa hiyo, hicho kijiji ambacho hakipo hatukutaja leo, kitaingizwa katika orodha ambayo itafuata.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wenye si mnaona, tunatakiwa kumaliza saa nne na nusu, tumechukua dakika kumi kwa sababu tulifanya zoezi la kuapisha Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, muda umekwisha na maswali yamekwisha.

Sasa naomba niwatambue wageni tulionao, kwanza kabisa nina wageni wa Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed, Mbunge ambaye tumemwapisha leo asubuhi nao ni ndugu Zena Abdulrahim na ndugu Hasna Masoud, hawa ni wake zake, walipo wanaweza kusimama, wako wawili pale. (*Makofii*)

Halafu yuko Mheshimiwa Ali Salum Haji, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi amemsindikiza na yupo Mheshimiwa Waride Juma, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi naye amemsindikiza na yupo ndugu yake mwingine Salum Bausa, wote mnakaribishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi karibuni, ndio ushirikiano mzuri tulionao. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Dokta Dalali Peter Kafumu, waliokuja kumsindikiza nayo ni familia yake Mheshimiwa Dokta Dalali Peter Kafumu, ikiongozwa na Mke wake Maria Magdalena Kafumu yuko wapi yeye, yuko hapa kwenye jukwaa la Spika, ameongozana na mtoto wake Dokta Imaculata Kafumu na yuko tena mtoto wake Dokta Kahesa Kafumu, hiyo nyumba ya Madaktari tupu, halafu yuko ndugu Benedict Kafumu mtoto wake mwingine, yuko Mary Kafumu, mtoto wake mdogo na yuko mtoto wake mdogo Janeth Kafumu. (*Makofii*)

Lakini pamoja na wao pia wamesindikizwa na ndugu wengine mmojawapo ni ndugu Masanja Kafumu kaka yake, yuko ndugu Tuma Kabata, mzee wa ukoo, yuko ndugu Felix Mkude, Mwenyekiti wa CCM. Hawakuniambia ni Wilaya ipi? (*Makofii*)

Halafu yuko ndugu Hyasinta Ngassa, yeye ni Mheshimiwa Diwani, yuko wapi Mheshimiwa Diwani na yupo ndugu yake Padre Joseph Maziku, Mwenyekiti Madhehebu ya Kikristo sijui ndio yuko wapi, ahsante. (*Makofii*)

Halafu yuko ndugu Shaila Ali Rage, Shekhe, wa Wilaya, wote wapo, ahsante karibu sana. (*Makofii*)

Hawa wazee hawa walitakiwa wakae pale kwenye *Gallery* ya Spika, bahati mbaya tu hatukuangalia vizuri, karibuni sana na tunawashukuruni kwa kazi nzuri mliyofanya ya uchaguzi uliohusika. (*Makofii*)

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara pamoja na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwa kutakuwa na kikao cha pamoja katika ya Kamati hizo leo tarehe 8 Novemba, baada ya kipindi cha maswali katika ukumbi wa *basement*, agenda ya kikao hiki ni kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya

Sheria Mbalimbali za Biashara. Naomba Wajumbe wa Kamati hiyo wote mfile kule muweze kushiriki katika kukamilisha Muswada ule.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo baada ya kipindi cha maswali katika Ukumbi namba 231 uliopo Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala, pia naomba hawa wajumbe waende kule wakashiriki.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 8 Novemba, saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa na Wajumbe wote wanaotakiwa kuhudhuria pia hii Kamati, naomba mkahudhurie.

Halafu nimepewa tangazo lingine na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa *caucus* ya Chama cha Mapinduzi, Bungeni, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM, kuhudhuria shughuli ya kuwapongeza Wabunge wapya leo saa saba, Ofisi za Chama, Makao Makuu saa saba. (*Makofî*)

Kutoka Ofisini kwangu natangaza kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi leo saa kumi na mbili jioni. Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wote kama Mwenyekiti hayupo, Makamu wake tutakuwa na kikao saa kumi na mbili jioni.

Sasa Waheshimiwa kama mtakavyoona *order paper* yetu, tumemaliza kwa maswali tu, hakuna shughuli nydingine yoyote, tunataka Kamati zikamalizie shughuli ambazo zinawahusu ili tuweze kuipanga ratiba yetu vizuri zaidi. Kwa hiyo, kuna Miswada kama miwili haikuwa imewekwa vizuri basi ikawekwe vizuri.

Lakini kuna Mheshimiwa mmoja hapa ameniandikia *note* yake anasema, yeye amepata kuulizwa na watu wengi pamoja na raia wa nje eti, vipi ninyi Watanzania kwenye Bunge lenu mnakanyaga bendera yenu ya Taifa, ameuliza Mheshimiwa mmoja hapa. Sasa hatukanyagi bendera ya Taifa, mkiangalia hapa kuna rangi za bendera ya Taifa lakini siyo bendera ya Taifa, bendera ya Taifa ina mpangilio wake. (*Makofî*)

Kwa hiyo ni rangi za bendera ya Taifa lakini siyo bendera ya Taifa, naomba ukiangalia vizuri na wanaoangalia pia waangalia bendera ya Taifa haipo namna hii lakini rangi zake ndiyo hizi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hilo ndiyo jibu sahihi kwa wote. Sasa naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 4.57 Asubuhi Bunge lillahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano,  
Tarehe 9 Novemba, 2011 Saa Tatu Asubuhi*)